

Shule 240 kufundishwa usalama

■ Ibrahim Yamola

SERIKALI inatarajiwa kuzipatia mafunzo ya usalama barabarani Shule za Msingi 240 za jijini Dar es Salaam.

Akizungumza kwenye uzinduzi wa Mafunzo ya Usalama barabarani yaliyofanyika katika Shule ya Msingi, Mnazi Mmoja, Ofisa Elimu ya Watu Wazima wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, Angelina Majinde, alisema mafunzo hayo yatasaidia kupunguza ajali zinazoepukika.

Alisema kutokana na hali hiyo wanafunzi watapatiwa mafunzo ambayo yatawasaidia kuelewa alama mbalimbali za barabarani pamoja na kujifunza jinsi ya kuvuka, jambo ambalo wanaamini linaweza kupunguza ajali hizo.

"Ajali nyingi zinazotokea jijini zinasababishwa na baadhi ya wananchi kutojua alama za barabarani wakiwamo wanafunzi, jambo ambalo limesababisha kuteua baadhi ya shule ili kuzipatia mafunzo hayo," alisema Majinde.

Alisema kutokana na hali hiyo watumiaji wa barabara wanapaswa kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali zinazosababisha vifo, ulemavu na upotevu wa mali.

Kwa mujibu wa Majinde, mafunzo hayo yatafanywa mara baada ya vipindi vya darasani ili kuepuka kutokukamilisha kwa mitalaa ya walimu wakati wa masomo.

Alisema kutokana na hali hiyo idadi kubwa ya wanafunzi wata-



TIBA: MAFUNZO

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mafunzo ya Tiba ya Magonjwa ya Tumbo, Dk John Rwegasha (kulia), akimweleza jambo Mkurugenzi Mtendaji wa Chuo Kikuu cha Philipps, Ujerumani, Profesa Rudolf Arnold (katikati) alipotembelea baadhi ya vitendea kazi vya mafunzo ya magonjwa ya mfumo wa chakula na ini yaliyoanza jijini Dar es Salaam jana. Mwingine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Tanzania Medical Equipment (TAMEQ), Alexander Riefer. Picha na Rafael Lubava.

'Matatizo lukuki kwa walemavu'

■ Maimuna Kubegeya

LICHA ya kupitishwa kwa sheria ya Watu Wenye Ulemavu Tanzania Bara ya mwaka 2010 na ile ya Zanzibar ya mwaka 2006, jamii ya watu wenye ulemavu, bado inakabiliwa na changamoto lukuki, zikiwamo ukosefu wa mazingira rafiki.

Mratibu wa Mradi wa Lugha ya Alama, unaofadhiliwa na 'The Foundation for Civil Society' kutoka Wilaya ya Dodoma, Ramadhan Kimolo alisema changamoto hizo zimekuwa zikichangia umasikini wa jamii ya watu wenye ulemavu.

Alisema jamii ya wenye ulemavu mara nyingi wanashindwa kuzifikia huduma muhimu zinazochangia maendeleo yao.

"Walemavu wengi wakiwamo wenye ulemavu wa kutosikia wamekuwa nyuma kimaendeleo, kutokana na kukosa fursa mbalimbali za kujiendeleza, jambo linalochangiwa na kuko-sekana kwa mazingira rafiki" alisema.

Alisema ni jukumu la Serikali kuhakikisha walemavu wanapata huduma stahiki kwa maendeleo yao na jamii kwa jumla.

Akizungumzia changamoto za walemavu wa kutosikia, Kimolo alisema miongoni mwa mahitaji makuu ya walemavu wa kutosikia ni ukosefu wa elimu ya lugha ya alama.

Alisema kutokana na kuto-

Wanafunzi 4,000 hawajafanya